# SHULE YA WASICHANA YA GATITU
## MTIHANI WA MUHULA WA KWANZA
## KIDATO CHA KWANZA 2016

**JINA……………………………………………………………DARASA…………..NAMBA…………..**

**1)SOMA TAARIFA IFUATAYO KISHA UJIBU MASWALI YANAYOFUATA**

**UCHAFUZI WA MAZINGIRA**

Mafuta yanayopatikana kwenye fukwe za bahari, moshi wa magari, takataka na bidhaa **nyinginezo** zilizotupwa hapa na pale ni vichafuzi vya mazingira. Vichafuzi huathiri afya zetu na kuwaathiri wanyama pamoja na mimea. Wanadamu wanachafua mazingira yao kwa kila aina ya bidhaa mbaya za kemikali zinazotoka viwandani au kwenye viwanda vya kawi au nguvu. Bidhaa hizo ni matokeo ya maisha ya siku hizi anayoishi binadamu.

Licha ya ukweli huu, ni muhimu kujua kuwa uchafuzi wa mazingira haukuanza leo. Miaka na miaka iliyopita, viwanda vimekuwa vikitoa mawingu makubwa ya moshi wenye sumu. Hata hivyo, uchafuzi wa mazingira umeongezeka <u>maradufu</u> kutokana na kuongezeka kwa viwanda. Uchafuzi <u>umesambaa</u> ardhini, kwanye anga na majini. Msambao huu unapatikana katika pembe zote za ulimwengu wetu. Je, kuna aina zipi za uchafuzi?

Kwanza kuna uchafuzi wa halianga. Huko juu angani kuna tabaka linalojulukana kama ozoni. Tabaka hili huwa ni aina ya gesi ya oksijeni Na linaunda kinga fulani dhidi ya miale ya jua. Miale hiyo ya jua huweza kusababisha kansa ya ngozi inapomfikia binadamu. Hata hivyo, uchafuzi wa mazingira unaelekea kuliathiri tabaka hili. Vili vile baadhi ya kemikali zinazotumiwa katika friji au jokofu, au kwenye mikebe ya marashi ya kupulizia na upakiaji bidhaa, huuharibu ukanda huo.

Aina nyingine ya uchafuzi ni ile tunayoweza kuiita uchafuzi wa kiajali. Huu ni uchafuzi ambao hutokea kama ajali, yaani binadamu hatendi kimakusudi. Mfano mzuri ni meli inayovuja mafuta baharini. Mafuta haya huwaathiri na kuwaua wanyama wanaoishi baharini kama samaki na ndege na hata kuyaharibu mazingira yenyewe.

Miji mikubwa hukumbwa na uchafuzi mwingine unaohusiana na kuwako kwa idadi kubwa ya magari. Magari haya hutoa moshi unaochanganya gesi ambazo huungana na nyingine zinazotolewa na viwanda vikubwa. Mchanganyiko huu unapoungana na maji, husababisha mvua ya asidi. Mvua hii huweza kuiua mimea, kuathiri majengo na hata kuwaua wanyama wa pori ambao huenda wakayatumia maji hayo. Magari hutoa moshiuliochanganyika na madini aina ya risasi ambayo huweza kuathiri siyo tu mazingira bali pia mfumo wa akili wa binadamu.

Uchafuzi mkubwa unaopatikana katika miji na mazingira mengine yetu ni utupwaji ovyo ovyo wa takataka. Fauka ya hayo, watu hufukia ardhini takataka ambazo huweza kuwa na matokeo mabaya kwa sababu ya <u>kupenyeza</u> kwenye udongo na maji yanayotumiwa na watu na mimea. Kila siku tunatupa takataka bila ya kujali wala kubali. Takataka hizi ni kama makopo,

mifuko ya plastiki, mabaki ya sigara au maganda ya matunda. Baadhi ya takataka ni hatari kwa wanyama na nyingine huweza pia kusababisha majanga kama moto. Aidha, takataka hizi huyafanya mazingira yetu yaonekane machafu.

Sote tuna jukumu kubwa la kuchangia kuupunguza uchafuzi wa mazingira. Hatua ya kwanza ni kuelimishana na kutambua umuhimu wa usafi wa mazingira yetu.Tunapaswa kutia takataka zetu katika vijalala maalum au mahali tunapoweza kuzichoma na kuziteketeza. Njia nyingine ni kuhakikisha kuwa tunatunza vitu kama mifuko, chupa na kadhalika ambavyo huweza kuundwa upya na kutumiwa tena. Hali kadhalika, katika miaka ya hivi karibuni, kumekuwapo na juhudi za kuwahimiza wenye magari kutumia mafuta ya gari ambayo hayana madini ya risasi. Kwa njia hii, tunasaidia kuyaboresha mazingira yetu. Vile vile pana umuhimu wa kutilia mkazo utumiaji wa bidhaa ambazo zinaweza kuoza na kuvunjikavunjika na kusagika na kuwa sehemu ya udongo.

Hatua ya kwanza ya kupambana na uchafuzi wa mazingira ni kujielimisha na kuwajibika. Kila mmoja akitoa mchango wake tutafanikiwa. Kumbuka kuwa kinga na kinga ndipo moto uwakapo.

Maswali

a)Andika vichafuzi vinne vya mazingiravilivyotajwa katika taarifa hii. (al. 2)

.............................................................................................................................

.............................................................................................................................

b)Ni madhara yapi yanayotokana na uchafuzi wa mazingira? (al. 3)

i)..........................................................................................................................

ii).........................................................................................................................

iii)........................................................................................................................

c)Eleza mambo mawili yanayofanya uchafuzi wa mazingira kuongezeka kila siku (al. 2)

i)..........................................................................................................................

ii).........................................................................................................................

d)Fafanua mambo manne anayofaa kufanya binadamu ili kuzuia uharibifu wa mazingira.(al. 4)

i)..........................................................................................................................

ii).........................................................................................................................

iii)........................................................................................................................

.............................................................................................................................

e)Ala za sauti zinaweza kuwekwa katika makundi mawili. Yataje. (al. 2)

i)..........................................................................................................................................

ii)........................................................................................................................................

f)Kamilisha jedwali lifuatalo (al. 3)

| konsonanti | aina | mahali pa kutamkia | ghuna/hafifu |
|---|---|---|---|
| p | .................................. | .................................. | .................................. |
| dh | .................................. | .................................. | .................................. |

g)Tambulisha nomino katika sentensi zifuatazo. (al. 2)

Uso wa Kaari umejaa huzuni baada kuanguka mtihani.

..........................................................................................................................................

h)Unda maneno yanayotokana na silabi hizi (al. 3)

i)silabi ya irabu moja ..........................................................................................................

ii)silabi ya konsonanti moja...................................................................................................

ii)silabi ya konsonanti tatu na irabu.....................................................................................

i)Onyesha mahali pa kuwekwa shadda katika maneno haya: (al. 2)

i)kiatu.........................................................................................................................................

ii)nzi..........................................................................................................................................

j)Eleza aina ya sentensi zifuatazo kwa kuzingatia kiimbo(al. 3)

(i)Amesema nini?....................................................................................................................

(ii)Waite watoto!.....................................................................................................................

(iii)Salaale! Gari limepita kama umeme....................................................................................

k)Onyesha vivumishi katika sentensi hii. (al. 2)

(i)Nyumba yangu inazungukwa na maua mazuri.

..........................................................................................................................................

(ii)Mti huu huzaa matunda mengi

..........................................................................................................................................

iv)........................................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................................

e)Andika methali moja iliyotajwa kwenye taarifa. (al. 1)

........................................................................................................................................................................

f)Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa kwenye taarifa. (al. 3)

i)maradufu..............................................................................................................................................

ii)umesambaa............................................................................................................................................

iii)kupenyeza.............................................................................................................................................

**2)MATUMIZI YA LUGHA**

a)maneno haya yanapatikana katika ngeli gani? (al. 5)

i)chakula..................................................................................................................................................

ii)ukuta....................................................................................................................................................

iii)maji.....................................................................................................................................................

iv)ugonjwa...............................................................................................................................................

v)mtume..................................................................................................................................................

b)Kanusha sentensi hizi (al. 2)

i)Wale watu wametoka ofisini.

........................................................................................................................................................................

ii)Paulo alifurahi kwa kumwona babake

........................................................................................................................................................................

c)Andika wingi wa sentensi ifuatayo (al. 3)

Shamba la mkulima yule limepandwa mbuni.

........................................................................................................................................................................

d)Taja irabu zifuatazo (al. 2)

i) ya kati inayotamkwa mdomo ukitandazwa. ........................................................................................

ii)ya nyuma mdomo ukiviringwa...............................................................................................................

l)Andika vitamkwa vya neon lifuatalo (al. 2)

nyuki..........................................................................................................................................................

**3 USHAIRI**

i)Shairi la mishororo mitatu huitwa.................................................................................... (al. 1)

ii)Jumla ya silabikatika mshororo huitwa.......................................................................... (al 1)

iii)Kipande cha kwanza katika mshororo ni......................................... na cha pili ni.........................

(al. 2)